KENYA LINK
K.I.3 SCHOOL BASED EXAM

KISWAHILI

DARASA LA 4
MUHULA WA III 2012

MUDA: SAA 1 DAKIKA 40

SOMA MAELEZO HAYA KWA MAKINI

1. Umepewa kijitabu hiki cha mas... na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali **50**

2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika kwa kijitabu hiki.

3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

4. Tumia penseli ya kawaida.

5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:-

JINA LAKO _____

JINA LA SHULE YAKO: _____

6. Kwa kila swali 1-50 majibu umepewa. Majibu A, B, C, D. Moja kati ya manne ni sahihi. Chagua jibu sahihi.

Mfano:
23. Tegua kitendawili kifuatacho: Ubwawa wa mwana mtamu
A. Usingizi B. Uji C. Maziwa D. Ndizi

Jibu sahihi ni **A (usingizi)**

Katika kijikaratasi chako cha majibu andika **nambari 22. (A)**

TURN OVER

KENYA LINK K.I 3 SCHOOL BASED EXAM
KISWAHILI DARASA LA 4 MUHULA WA 111 2012

Hospitalini ni mahali _1_ kuwatibu watu _2_ magonjwa mbalimbali. Hospitali _3_ huitwa _4_ au kituo _5_ afya. Daktari na mwuguzi hupatikana _6_ hospitali. _7_ ndio huwatibu wagonjwa. Vyumba vya _8_ wagonjwa huitwa _9_. Vifaa _10_ hospitalini huwa safi sana.

1. A. ya B. pa C. za D. wa

2. A. yenye B. zenye C. wenye D. nwenye

3. A. dogo B. mdogo C. kidogo D. ndogo

4. A. bweni B. chekechea C. zahanati D. nyumba

5. A. cha B. ya C. wa D. za

6. A. kwa B. na C. kwenye D. ndani

7. A. yeye B. nyinyi C. huyo D. wao

8. A. kuwalaza B. kuwalea C. kulia D. kuweka

9. A. darasa B. kodi C. wodi D. chumba

10. A. za B. ya C. vya D. la

Kutoka swali la 11 - 30 chagua jibu lifaalo zaidi

Andika wingi

11. Chumba hiki nitakifagia mimi
    A. Chumba hivi nitavifagia sis
    B. Vyumba hivi nitavifagia sisi
    C. Vyumba hivi nitavifagia mimi
    D. Vyumba hivi tutavifagia sisi

Andika umoja

12. Viazi hivi vimeliwa na wageni hao
    A. Viazi hivi vimeliwa na mgeni huyo
    B. Kiazi hiki kimeliwa na mgeni yule
    C. Kiazi hiki kimeliwa na mgeni huyo
    D. Kiazi hiki kimeliwa na mgeni huo

Andika kwa maneno

13. Magari 7,694
    A. Magari mia saba sitini na tisini na nne
    B. Magari elfu saba mia sita tisini na manne
    C. Magari elfu saba mia tisa sitini na manne
    D. Magari elfu saba mia sita tisini na nne

Jaza pengo

14. Sijamwona simba _____ macho yangu
    A. na B. kwa C. kama D. pamoja na

15. Kwaheri tuonane siku
    A. nyingine B. zingine C. ingine D jingine

16. Jaza A na B



    A. Kaskazini, Mashariki
    B. Kusini, Mashariki
    C. Magharibi, Kusini
    D. Kaskazini, Magharibi

17. Jua huchomoza kutoka upande wa
    A. Kusini B. Magharibi C. Mashariki D. Kaskazini

Malizia methali

18. Hasira _____
    A. Furaha B. Uzuni C. Hasara D. Hasira

19. Bandu bandu huisha
    A. Nyumba B. Gogo C. Kitabu D. Yote

20. Chai ya mkandaa ina rangi _____
    A. nyekundu B. zambarau C. hudhurungi D. urujuani

21.
    Mchororo huu wa mwandame _____
    A. hiramu B. tao

C. hirali D. nusu duara

22. Wakati kati ya adhuhuri na jioni huitwa _____?
A. asubuhi B. alfajiri
C. alasiri D. machweo

23. Mtoto wa paka ni _____
A. kiyoyo B. kivurumbi
C. kisui D. kipusi

24. Kaka wa mama ni _____
A. mjomba B. amu
C. shangazi D. angoo

25. Ni mnyama pia pia ni mtu anayesatisha vyoo. Huyu ni
A. dobi B. chura
C. kiboko D. nyani

26. Tulianika asubuhi saa moja na nusu. Hizi ni saa _____?
A. 12.30 B. 2.45
C. 7.30 D. 1.30

27. Mmea unaozaa kahawa huitwa _____?
A. mbuni B. mhindi
C. Mparachichi D. Mkahawa

28. Kamilisha misemo
Alipiga ____ kwa sababu alikuwa na uchovu mwingi na homa
A. mbio B. chafya
C. gumzo D. lami

29. Taja ngeli za nomino zifuatazo
Kalamu _____
A. I - I B. A - KA
C. I - ZI D. LI - YA

30. Majiko
A. YA - YA B. LI - YA
C. MA - MA D. MA - MA

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo

Nchi yetu ya Kenya ina mbunga nyingi za wanyama. Mbuga hizi zinapatikana katika sehemu mbalimbali za Kenya. Mojawapo ya mbuga hizi ni Tsavo. Mbuga ya wanyama ya Tsavo imengawanywa katika sehemu mbili. Kila sehemu iko chini ya waangalizi wa afisa wa kulinda wanyama.

Watu wanaotaka kuwaona wanyama wa porini hutembelea mbuga za Tsavo. Katika mbuga ya wanyama ya Tsavo kuna ndovu wengi. Watu hawa huitwa watalii.

Katika Tsavo ya magharibi kuna sehemu muhimu inayoitwa 'Mzima springs' na vidibwi vingi vya maji baridi ambamo viboko huishi. Pia kuna mahali mahalumu panapoitwa 'salt lick' ambapo wanyama huenda na kuramba chumvi Tsavo ya mashariki ni kubwa kuliko Tsavo ya magharibi katika sehemu nyingine za mbuga hii watu hawaingii bila kuongozwa.

katika mbuga hii kuna hoteli za kisasa za kuhudumia watalii.

31. Katika hadithi hii tumetaja wanyama wangapi?
A. Mmoja B. Watatu
C. Wawili D. Safuri

32. Mbuga ya Tsavo imegawanywa sehemu mbili na nini?
A. Mto mkubwa B. Barabara kuu
C. Msitumkubwa D. Maji mengi

33. Taja sehemu mbili za mbuga ya Tsavo
A. Magharibi na Mashariki
B. Mashariki na Kusini
C. Magharibi na Kaskazini
D. Kusini na Mashariki

34. Watu wanaotaka kuwaona wanyama wanaitwa aje?
A. Wananchi B. Watalii
C. Wazalendo D. Wakristo

35. Ni Tsavo gani kubwa kuliko nyingine?
A. Magharibi
B. Mashariki na Magharibi
C. Mzima springs
D. Mashariki

36. Watalii hutembelea mbuga za
A. Salt lick B. Tsavo
C. Mzima springs D. Magharibi

37. Sehemu za Tsavo Magharibi ni
A. Lango kuu la Tsavo
B. Salt lick na mzima springs
C. Hoteli za kisasa
D. Pori ya Tsavo

38. Kulingana na hadithi hii, viboko huishi kwenye
A. Hoteli B. Barabara
C. Vidibwi vya maji D. Tsavo

39. Hoteli nyingi za Tsavo hutumika kwa kuwahudumia
A. Watoto B. Wanyama
C. Wasafiri D. Watalii

40. Neno vidibwi limepigwa mstari, maana yake ni
A. Shimo la maji B. Mchezo
C. Shamba D. Lango la kuingilia

Soma makala haya kisha ujibu maswali 41 - 50

Tofauti gani ya mimi na wewe? Nakupenda vangu. Nakuonea imani unadhulika, unateseka na ulimwengu na hata hujali. Paka umezaliwa, unakula nini? Unavaa nini? Nakufunga mimi bwana yako au nakudhalilisha? Ikiwa unahisi nakutesa maana sikupi chakula, sikupi nguo, sikupi pahala pazuri pa kulala. Sikupi vyote kwa sababu mimi mwenye sinavyo. Mimi mwenyewe navihihitaji, usilie paka wangu. Usione unyonge kwani watu wana kuhusudu, wewe kuzaliwa paka. Mimi mwenyewe nakuhusudu mara ngapi nimetamani laiti wewe ungalikuwa mtu na mimi nikawa paka. Ungaliwezaje kunilisha?

Nje, ungalinivisha? wewe bora, paka, bora wewe paka wangu. Namimi paka, paka kasoro mkia..

41. Badala ya kusema, "Tofauti gani ya mimi na wewe?"
Pia angesema, "Tofauti gani _____ mimi na wewe?"
A. Kwa B. Kati kati
C. Mwa D. Kati ya

42. Nakuonea imani ni kusema
A. Nakusikilia huruma
B. Nakuonea huruma
C. Nakuhurumia
D. Nasikia huruma na wewe

43. Majaliwa hutoka kwa
A. Paka B. Dude
C. Mungu D. Mti

44. Dude hampi paka mahitaji yote kwa sababu
A. Hana B. Hataki
C. Hapendi D. Paka hali

45. Kiswahili mufti ni sikupi. Ni makosa kusema
A. Sikutolei B. Sikupatii
C. Sikupei D. Sikungawii

46. Tunasema nikawa paka. Wasiojua Kiswahili mufti husema
A. Nikangeuka B. Nikakuwa
C. Nikabandilika D. Nikangeuzwa

47. Ungalinivisha. Neno visha hutokana na kitenzi
A. Via B. Faa
C. Ma D. Vaa

48. Dude ambaye ni mwenye paka ni mtu
A. Maskini sana B. Tajiri sana
C. Mvivu sana D. Mbaya sana

49. Neno paka limetajwa mara ____ katika ufahamu
A. Tisa B. Kumi
C. Saba D. Nane

50. Laiti lina maana sawa na
A. Vile B. Kama
C. Sivyo D. Hama

Printed by: Lauh Print Company Limited P.O. Box 2015, Tel: 044-20405,0733235770-Machakos.